JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI

MAWAZIRI WA FEDHA WA AFRIKA WAZUNGUMZIA MIKISIKO WA UCHUMI

Wakizungumza na waandishi wa habari mjini hapa Washington DC, Mawaziri wa fedha kutoka nchi ya Cameroon, Jamhuri ya watu wa Congo, Liberia na Uganda, kila Waziri aliongelea jinsi mtikisiko huo ulivyo waathiri. Bw. Essimi Menye ambaye ni Waziri wa Fedha wa Cameroon alisema kuwa, mtikisiko huo umewakumba zaidi watu wenye kipato cha chini kwani wao hutegemea sana kuuza bidhaa ambazo zinatokana na misitu na kilimo. Sasa imewaathiri kwni soko hilo lilishuka.

Waziri huyo wa Cameroon aliendelea kueleza kuwa kwa zile Nchi zinazouza malighafi kama vile mafuta zimepata shida hiyo kwa ajili ya mabadiliko ya bei, lakini pamoja na hayo yote tumejitahidi kulipa madeni yetu japo bado kuna mengine tunatakiwa tuyalipe.

"Jambo kubwa la muhimu ni deni letu kwa sababu pato letu ni dogo na deni linazidi kukua. Bila shaka tunahitaji kuwa na fedha na kuhakikisha shughuli za serikali zinaendelea, tunapaswa kulipia bidhaa zinazonunuliwa". Menye alisistiza.

Aidha aliendelelea kusema kuwa pamoja na kuwa na kiwango cha mapato ambayo hayajabadilika kwa sababu ya uzalishaji kutokuongezeka, imetusababishia matatizo makubwa katika nchi yetu. Tulikuwa tunafikiri kuwa tufike mahali haya mambo ya kamilike kwakuhakikisha kuwa uzalishaji unaongezeka na hata pato la Serikali linaongezeka. Hiki ndicho kitu ambacho nilikuwa nataka kukitilia mkazo".aliseama Menye.

Wakati huo huo naye Waziri wa Fedha wa Kongo Bw. Ondongo aliwaeleza waandishi wa habari kuwa, tatizo la kifedha halijaigusa nchi yake ya Congo,kwa sababu nchi yake haina mfumo wowote wa fedha ambao unawawezesha wao kuwa na muingiliano wa kimapato pamoja na athari na nchi zenye pato la juu.

"Kwa upande wa uchumi , tumeathirika hasa katika uuzaji wa bidhaa hizi mbili ambazo ni Mafuta na Mbao.Shughuli zetu zinazohusiana na mbao na Miti zimeathirika sana zaidi ya mafuta" aliongea kwamasikitiko. Uzalishaji wa Mbao umepungua kwa zaidi ya mita za mraba 1,300,000 tangu 2008.Na mauzo ya nje pia yamepungua kutoka mita za mraba bilioni 1 mwaka 2008 mpaka mita za mraba 420,000 kwa mwaka 2009, hii ina maanisha kuwa yameshuka kwa asilimia 60".alieleza Menye.

Aidha Bw.Menye alisema kuwa sekta ya mbao ndio inaongoza kwa kuajiri watu lakini kwa hapa inaonekana inachukua nusu ya watu. Aliendelea kueleza kuwa, tatizo tunalolipata ni kuwa Congo tumezoea kuuza mbao kwenye nchi za Ulaya, hasa ureno na Spain, hawa ndio wanaonunua mbao hizi kwa ajili ya ujenzi.

Kwa upande wa mafuta ni kwamba kushuka kwa bei kumeufanya uchumi wa Congo kuharibika. Bei imeshuka kutoka dola za kimarekani 150 mwaka 2008 mpaka dola za kimarekani 40 mwishoni mwa mwaka 2008. Kwa hiyo hii imetulitea matatizo sana katika uchumi wetu ambao kama mnavyo jua kuwa unategemea mafuta . Asilimia 80 ya pato letu linatokana na mafuta . Asilimia 70-75 ya pato la ndani la Taifa linategemea mafuta. Asilimia zaidi ya 90 ya mauzo yetu nje ni mafuta.Kwa kutokana na haya pato letu limekatwa katikati, kutoka dola za kimarekani bilioni4 ya pato hadi chini ya dola za kimarekani bilioni 2 mwaka 2009 hii ni kwa sababu ya huu mtikisiko.Menye alieleza.

"Pamoja na yote hayo uchumi wa Congo hauja tikiswa sana. Mwaka 2008 uchumi wetu ulikua kwa zaidi ya asilimia 5. Na mwaka 2009 ukuaji wa uchumi umekuwa wa mafanikio,maana umekuwa kwa zaidi ya asilimia 6, asilimia 6.2. Na hii nikutokana na kuwa na uchumi imara kwenye nchi yetu". alijigamba waziri huyo.

"Tunashukuru ushirikiano wetu na Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki ya Dunia kwa kutuwezesha kuuweka upya uchumi wetu. Tumeweza kutengeneza ukweli na uaminifu wa ndani unaoeleweka na Sekta ya simu za mikononi, na hata Sekta nyingine pia.Hii imetusaidia kutukinga na huo mtikisiko na vilevile inatuandaa kwa maisha bora ya baadae. Kutokana na maoteo ya Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki kuu za nchi zetu ni kwamba tunategemea uchumi kukua kwa kiwango cha asilimia 13, kiwango ambacho ni kizuri na cha juu katika Afrika".alieleza Menye.

Naye Waziri wa Liberia Bw. Ngafuan alizungumza na waandishi wa habari kwa kuwaambia kuwa ninatoka Liberia, nchi ambayo imekuwa na mapigano kwa zaidi ya miaka 14 na mapigano hayo yamesababisha vifo vya watu zaidi ya 200,000, mabarabara yameharibiwa na kila kitu kitu kimeharibika na ili vitengenezwe kunahitajika nguvu ya ziada.

" Mwaka 2006 Rais wetu , Madam Ellen Johnson Sirleaf, alianza kuutengeneza uchumi upya kwa kutumia timu ya watunga sera za

uchumi na kuwaweka wananchi wake katika hali ya kuwa na nidhamu kifedha na kuachana na vita. Kwa hiyo matatizo haya ya kupungukiwa na chakula, mafuta na uhaba wa fedha haukuja katika wakati mbaya kwa nchi yangu. Tulikuwa tumeshaanza kunyanyuka na kuondoka lakini hii hali imetufundisha mengi katika kuwa makini na kufanya mabadiliko yanayoangalia ukuaji wa uchumi wetu.Katika mkakati wetu wa miaka 3 wa kupunguza madeni,tulitegemea uchumi kukua kwa asilimia kama 12 kati ya mwaka 2008 mpaka 2009.Lakini mtikisiko umefanya ukuaji huo kupungua kwa asilimia 5, kiasi kwamba imetulazimu kupunguza matumizi yetu na matumizi ya deni la ndani".alisisitiza Menye.

"Tumerithi mzigo wamadeni makubwa,deni letu kwa kwa uwiano wa pato la ndani lilikuwa zaidi ya asilimia 700. Kwa hiyo Liberia imekuwa kwenye sehemu ya nchi zenye madeni makubwa.Tumefikia kwenye hatua ya maamuzi, na sasa hivi tunatumia kadiri tunavyopata tofauti na nchi nyingine kwa sababu hatukua na jinsi. Nafikiri ni nchi yetu pekee hapa Duniani ambayo wana nchi wake wanaishi kwa kutegemea makusanyo yetu ya kodi. Na kama tukipungukiwa na makusanyo ya mapato tunachokifanya ni kuondoa matumizi yasiyo ya lazima. Kwa hiyo hili limekuwa nitatizo kwa Liberia". aliongeza Menye.

Aidha aliendelea kueleza kuwa,wanatambua kuwa kitu kinachowafanya wa Liberia kuwa katika deni kubwa ni kukosa nidhamu ya kifedha kwa hiyo walichokifanya sasa ni kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha. Ni hivi punde tu Shirika la fedha la kimataifa lilikuwa likipitia na kuangalia deni letu nafikiri kama tutakuwa tunaenda vizuri itatusaidia kujua jinsi ya kumaliza deni hilo.

Menye alisema kuwa "Mtikisiko umeathiri sekta zinazouza vitu nje, Liberia tunauza sana Mikonyo(Raba). Mwaka 2008 makadirio ya kuuza nje Raba yalikuwa milioni 242.Baada ya mtikisiko ikashuka hadi kufikia milioni 152. Wafanyakazi katika sekta hizo walipoteza kazi pia hata katika sekta za madini.Kuna kampuni moja kubwa ambayo inaitwa Arcelor Mittal, ilikuwa ianze kuuza chuma kutoka Liberia mwaka huu lakini kwa sababu ya haya matatizo imeahirisha mpango wake hadi mwisho mwa mwaka 2011 na hiyo nayo imesababisha wafanyakazi kupunguzwa kazi".

"Kipindi tulicho kuwa tunahangaika na ukosefu wa ajira kwa vijana tulikuwa tuna kitu tunakiita vita ya vijana na ikatufikisha kwenye vita kweli.Hii ina niogopesha sana. Tunategemea kila mshirika wetu anapambana ili kuhakikisha hali hii haitokei tena. Kwa sababu tunatakiwa kuhakikisha kuwa watu wetu wanapata kazi kwa sababu kukosa kazi sio tu kunapoteza usawa bali pia amani ya nchi yetu inapotea. Sisi ni nchi maskini na ndio kwanza tumetoka kwenye vita kwa hiyo kukosa kazi kumeweka mazingira ya woga". alieleza Ngafuan.

"Tunapaswa pia kujiingiza kwenye ujenzi wa miundo mbinu kama vile

kujenga barabara, bandari, na miundombinu mingine.Vilevile tunahitaji kuwa na mpango kazi wa serikali kwa kufanya mabadiliko ya muundo serikalini, kitu ambacho tumekuwa tukikifanya tangu mwaka 2006. Tumeiimarisha ofisi yetu ya kamishna mkuu wa ukaguzi wa fedha , tumeiimarisha ofisi ya mwanasheria Mkuu, na tumeiimarisha ofisi ya kupambana na rushwa na tuna mfumo wa Bajeti ulio wazi.Kwa hiyo ningependa niwaambie kuwa mtikisiko huu haukuja katika kipindi kibaya kwa Liberia ila wakati unakuja ndio tulikuwa tumejiandaa kunyanyuka kiuchumi.Lakini tunashukuru kwa kuwa na uongozi mzuri na mipango mizuri ya uchumi,na timu zinazoshughulikia mambo ya fedha kama mabenki na watendaji wa serikali , maana tumeweza kupambana na huo mtikisiko". Aliongea waziri huyo.

Naye waziri wa fedha wa Uganda Bi. Bbumba aliwaambia waandishi wa habari kuwa mtikisiko uliotokea huko Uganda ulikuwa na athari ndogo sana hii ni kwa sababu ya mipango mizuri ya kifedha na uongozi mzuri katika matumizi ya fedha hizo.Vilevile ni kwa sababu sekta zakifedha haizikuunganishwa. Tumepata shida kidogo tu kwenye fedha za kigeni hii ni kwa vile kulikuwa na tatizo kwenye kuuza bidhaa nje.Ni lazima tupate matatizo haya kama nchi za ulaya zinapata matatizo kwani wawekezaji wengi wanatoka Ulaya na hii ina sababisha hela zinazoingia kupungua.Kuna kampuni kubwa za ndege zilibidi ziondoke ili kujiokoa katika kupoteza fedha zao hiyo imesababisha tatizo katika sarafu zetu.

Tuna waganda wengi ambao wanafanya kazi nje ya nchi , makato yao ya fedha zinazokuja kwetu yamepungua kwa sababu ya hayo matatizo katika sehemu zao za kazi. Na hizo fedha zinasaidia sana katika ujenzi wa Taifa letu la Uganda. Kumekuwa na kuongezeka kwa bei ya vitu na sarafu zetu kushuka thamani,hii imesababisha kukimbia kwa tunaofanya nao biashara.

Baadhi ya wauzaji na wanunuaji wa bidhaa nje ya nchi wameathirika, lakini sio sana ila kwa wauzaji wa maua.Hii imeathiri mapato yetu.Pamoja na kuwa mapato yetu yamekuwa chini kwa asilimia 10 hii ni chini ya lengo tulilojiwekea,lakini bado ni kiwango cha juu kwa kiwango tulicho kusanya mwaka uliopita.

Hivyo basi napenda kuwaambia athari zilizotokea ni ndogo sana lakini kikubwa tunacho kiangalia ni biashara ya pamojana nchi jirani.Ila nashukuru kwa waliochelea kufanya biashara na sisi, hii imetufanya tuangalie jinsi ya kufanya biashara katika soko la pamoja na nchi jarani hasa katika bidhaa za chakula, hii itatusaidia kufanya biashara kila siku. "Na hakika hii imetufumbua macho, Sasa tunatilia mkazo biashara ya kilimo na nchi jirani. Kabla ya haya matatizo watu walikuwa wanalima kiasi kinacho watosha wao tu,na kiasi kidogo sana cha kuuza lakini sasa

tumekuja na sheria kali inayo hakikisha kuwa kila kaya inadhalisha zaidi ya wanachokitumia na waweze kuuza kiasi kingine kwenye soko la pamoja."alieleza Bbumba

Bbumba aliendelea kusema kuwa"nafikiri hii itaonyesha vilevile umuhimu wa kuwa na soko la pamoja ambapo tutafanya biashara bila vipingamizi vyovyote kwa sababu biashara kubwa itafanyika katika jumuiya ya Afrika mashariki ambapo tuko katika hatua ya mwisho ya kumalizia mchakato huo wa kuwa na soko la pamoja.Nafikiri hiki ni kitu muhimu sana kwa Afrika. Kabla hatuja fanya biashara na nchi za mbali hembu tutumie nafasi hii kufanya sisi wenyewe kwanza". Tumekuwa na matatizo ya kupungukiwa na mafuta, hili ni tatizo la muda tuna mategemeo mazuri kwani Uganda inategemewa kuwamojawapo ya nchi zinazozalishamafuta.

"Pamoja na yote hayo tumeweza kukabiliana na huu mtikisiko , lakini kitu cha muhimu ni ule ushauri na misaada tuliyokuwa tunapewa na washirika wetu kama Shirika la fedha la kimataifa , wakopeshaji wetu, wafadhili kama Benki ya Dunia na wengine, bila huo msingi imara tusingeweza kuwa katika hali hii ukizingatia kuwa sisi ni nchi masikini, na si muda mrefu tumetoka kwenye vita.alieleza Waziri huyo.

Mawaziri hao wa Fedha kutoka Afrika ambao walikuwa na mkutano na waandishi wa habari kila mmoja aliweza kuielezea nchi yake na jinsi ilivyoathirika kutokana na mtikisiko huo wa uchumi ulioikumba Dunia mwaka jana, mawaziri hao ni pamoja na Essimi Menye kutoka Cameroon,Gilbert Ondongo kutoka Congo, Augustine Ngafuan kutoka Liberia, na Syda Bbumba kutoka Uganda.

Imetolewa na Msemaji Mkuu
Wizara ya Fedha na Uchumi
Washington DC
24/04/2010